# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua Pepe: ps@mit.go.tz
Barua Pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S.L.P 2996,
**40478, Dodoma**.

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## KAMATI YA KUFUATILIA NA KUHAKIKISHA RAIA WA KIGENI HAWAJIHUSISHI NA BIASHARA ZINAZOPASWA KUFANYWA NA WAZAWA KARIAKOO

**02/02/2025, DAR ESSALAAM.**

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.) ameunda Kamati ya Wajumbe kutoka Taasisi mbalimbali za umma na binafsi itakayofanya kazi kwa siku 30 kwa ajili ya kufuatilia na kuhakikisha raia wa kigeni hawajihusishi na biashara zinazopaswa kufanywa na Wazawa jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa na Wafanyabiashara Wazawa.

Waziri Jafo ameunda Kamati hiyo ikiwa ni utekelezaji wa Maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu kuhakikisha raia wa kigeni hawajihusishi na biashara zinazopaswa kufanywa na Wazawa, kufuatilia utoaji wa leseni za biashara kwa Wazawa na wageni ikiwa ni pamoja na kusajili wafanyabiashara na kuwa na kanzidata yao

Wajumbe wa Kamati hiyo iliyoundwa kutekeleza maelekezo hayo ni kama ifuatavyo:

i) Prof. Edda Tandi Lu,oga, Mkuu wa Chuo cha Biashara (CBE) – Mwenyekiti;
ii) Bw. Sempheo Manongi Nyari, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, Wizara ya Viwanda na Biashara – Katibu;
iii) Bw. Francis Marco Maro, Naibu Kamishna wa Polisi – Mjumbe;
iv) Bi. Kigongo Shile, Naibu Kamishna wa Uhamiaji - Mjumbe;
v) Bi. Latifa Khamis Mohamed, Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE) - Mjumbe;
vi) Bw. Gilead John Teri, Mkurugenzi Mkuu, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) – Mjumbe;
vii) Bw. Godfrey Nyaisa, Mtendaji Mkuu, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) – Mjumbe;
viii) Bw. William E. Erio, Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani (FCC) – Mjumbe;
ix) Bw. Ted Frank Silkiluwasha Kamishna Huduma za Ufundi, Idara ya Kodi za Ndani, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Mjumbe;

x) Bi. Zubeda Masoud, Katibu Tawala Msaidizi - Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mkoa wa Dar es Salaam – Mjumbe;

xi) Lilian Denis Francis, Kamishna Msaidizi-Vibali vya Kazi, OWM - Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu – Mjumbe;

xii) Bw. Elihuruma Mabelya, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam – Mjumbe;

xiii) Bw. Raphael Maganga, Afisa Mtendaji Mkuu, Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) - Mjumbe;

xiv) Bw. Hamisi Livembe, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania – Mjumbe;

xv) Bw. Severin Mushi, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo – Mjumbe; na

xvi) Bw. Leonce Bilauri, Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Itifaki, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa – Mjumbe.

Wajumbe wa Kamati hiyo wataongezwa kwa kadri ya mahitaji yatakayobainika.

**Imetolewa na:**

**Suzan C. Mshakangoto**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Viwanda na Biashara